# TNMC Habari

Toleo No. 0013

TOLEO MAALUMU

Septemba, 2024

HALIUZWI

www.tnmc.go.tz @tnmchabari




## TNMC Yashiriki Mkutano wa ECSACON Lesotho

Habari Uk. 02



## Tanzania Yapiga Hatua Sekta Ya Afya

Habari Uk. 03

TUNABORESHA AFYA
MTU NI AFYA • AFYA NI MTAJI

# Kamati ya Bunge ya Afya, Ukimwi Yapokea Taarifa ya Baraza la Uuguzi na Ukunga



Habari Uk. 01

## MCT na TNMC wabadilishana Uzoefu Uendeshaji Mitihani ya Usajili, Leseni

Habari Uk. 06

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlakaya Kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 na kanuni zake (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

# TIMU YA WAHARIRI


## MWENYEKITI

Bi. Agnes Mtawa

## MHARIRI

Mwakapiso Ndimmyake

## WARATIBU

Irene Chilewa

Rose Mhando

## MSANIFU JARIDA

Ezekiel Nyalusi



P.O BOX1736 DODOMA

TEL.022-212133975 Fax.022-2133975 Mobile:0786785947

# TNMC Yawasilisha Taarifa Ya Utendaji Kazi Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Mbele Ya Kamati Bunge.



**Na. Ndimmyake Mwakapiso**

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga nchini Tanzania Bi. Agnes Mtawa, akiwa ameambatana na menejimenti yake, tarehe 06 Agosti 2024 amewasilisha taarifa ya utendaji kazi ya Baraza kwa mwaka wa fedha 2023/2024 mbele ya kamati ya Bunge inayosimamia sekta ya Afya na UKIMWI kupitia kikao kilichofanyika katika ukumbi mdogo wa Bunge Jijini Dodoma.

Kamati inayoongozwa na Mwenyekiti Mhe. Elibariki Kingu (MB) na wajumbe 15, kwa ujumla wamefurahishwa na wasilisho la Msajili na kubainisha kuwa wasilisho hilo limetoa uelewa wa kutosha kwa wabunge wa kamati hiyo kwa kulifahamu kiundani Baraza pamoja na mipango yake.

Wasilisho la msajili kwa kamati lililenga mambo muhimu ikiwa ni pamoja na utangulizi wa kulifahamu Baraza, Dhima na Dira, Muundo wa Baraza, Majukumu yake, usajili wa wanataaluma, Umuhimu wa wauguzi kujiendeleza wakiwa kazini CPD, uwepo na umuhimu wa Mtihani wa usajili na leseni pamoja na mafanikio ya Baraza tangu kuanzishwa kwake mwaka 1953.

*"Kwa kweli tuwapongeze sana Baraza kwa utendaji mzuri wa kazi, wabunge wamefahamu nakuelewa vitu vingi kuhusu Baraza hili muhimu na pia nikupongeze sana Msajili Dada Agnes, kwa kweli unaonesha jinsi gani unaijua taasisi unayoiongoza, CMO huyu ni hazina ya Wizara ya Afya endeleeni kumtumia kwa mambo mengi"* Alisema Mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Elibariki Kingu.

Aidha, baada ya wasilisho hilo wabunge ambao ni wajumbe wa kamati hiyo, waliuliza maswali mbalimbali yenye nia ya kujenga uelewa zaidi na maswali yote yalijibiwa vema



# TNMC Yashiriki Mkutano wa ECSACONM Lesotho




## Na. Mwandishi Wetu

TNMC ikiwakilishwa na Msajili Baraza la Uuguzi na Ukunga Bi. Agnes Mtawa, pamoja na maafisa waandamizi ambao ni Salome Kassanga kutoka kurugenzi ya Usajili, leseni na maadili ya kitaaluma pamoja na Bi. Irene Chilewa, ambaye ni Mkuu wa kitengo cha uthibiti ubora, imeshiriki Mkutano wa kimataifa wa kisayansi unaoratibiwa na Jumuiya ya ECSACONM nchini Lesotho kuanzia tarehe 11 hadi 13 Septemba 2024 kwa lengo la kubadilishana elimu, uzoefu na kuboresha utoaji huduma katika sekta ya Afya kwa nchi wanachama.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano huo, Rais wa jumuia ya ECSACONM Dkt. Glory Msibi, amewakaribisha wajumbe wa mkutano huo na kutanabaisha kuwa mkutano huo ni muhimu katika kuendeleza taaluma ya Uuguzi na Ukunga kwa ukanda wa Afrika mashariki na kati na kusini mwa Afrika.

***"Mkutano huu utakaofanyika kwa siku hizi tatu, unatupa fursa ya kutafakari, kusherekea na kushirikishana mikakati, uvumbuzi na maarifa na kuimarisha utendaji wetu"***

Mkutano wa ECOSACONM unaotoa fursa kwa washiriki kujifunza, kufahamiana na kubadilishana uzoefu katika utoaji wa huduma za Afya, uelimishaji wa Uuguzi, Wadhibiti, Serikali na vyama vya kitaaluma, huandaliwa katika nchi mbalimbali wanachama ambapo Tanzania ni miongoni mwa nchi hizo.



ECSACONM ilianzishwa mwaka wa 1990 kama chombo cha utekelezaji cha iliyokuwa Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini (CRHCS-ECSA) katika eneo la Uuguzi na Ukunga chenye makao yake makuu Jijini Arusha nchini Tanzania, ambayo sasa inajulikana kama Jumuiya ya Afya ya ECSA (ECSA HC) ikiwa na majimbo 14 ya kikanda. Pia, ni mojawapo kati ya vyuo vitano vya ECSA-HC ambavyo ni COSECSA ,CANECSA, COPECSA na ECSACOG.

Jumuiya ya nchi wanachama 18 ambazo ni Tanzania, Botswana, Kenya, Lesotho, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Rwanda, Seychelles, Afrika Kusini, Sudan Kusini, Swaziland, Uganda, Zambia Zimbabwe, Ethiopia na Madagasca

# Tanzania Yapiga Hatua Sekta ya Afya - Waziri Mhagama

**Na. Mwandishi wetu**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepiga hatua kubwa katika Sekta ya Afya kwa kudhibiti maabukizi ya VVU, TB, Malaria, mifumo ya Afya iliyostahimilivu na endelevu pamoja na kuboresha utendaji wa kazi kwa watumishi.

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amesema hayo leo Septemba 12, 2024 wakati wa kikao cha pamoja na Mkuu wa Idara, High Impact 2 wa Global Fund Bw. Linden Morrison, kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Afya Jijini Dar Es Salaam.

*"Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa msaada mkubwa wa kifedha na kiufundi unaotolewa na Global Fund, kwa miaka mingi msaada huu umetuwezesha kupata maendeleo makubwa katika kudhibiti VVU, TB na Malaria huku pia tukijenga mifumo ya Afya iliyostahimilivu na endelevu."* Amesema Waziri Mhagama



Aidha, Waziri Mhagama amesema kupitia uimarishaji wa afua za kuzuia na kuongezwa kwa huduma na matibabu, maambukizi mapya ya VVU na vifo vinavyohusiana na UKIMWI vimepungua ambapo Tanzania imepata maendeleo makubwa kuelekea malengo ya 95-95-95, ambayo kwa sasa yanasimama katika 83-98-94.

Amesema, kwa sasa mifumo ya Afya imeimarika kwenye vituo vya Afya pamoja na mifumo ya Afya ya jamii ambapo Tanzania imejiandaa kukabiliana na magonjwa ya milipuko endapo itatokea nchini.

*"Serikali imepiga hatua katika utunzaji wa watoto wachanga kwenye vituo 523 vya huduma ya dharura ya Uzazi (CEMOC), tunaomba usaidizi wa kuanzisha vitengo vingine zaidi ili tuweze kuokoa maisha ya watoto hao pamoja na usaidizi wa kifedha kwa ajili ya kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na magonjwa ya milipuko ikiwemo wa Mpox."* Amesema Waziri Mhagama.






# TNMC ,MCT Wabadilishana Uzoefu Kuhusu Uendeshaji Mitihani ya Usajili na, Leseni



Na. Mwandishi wetu

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) kupitia Kurugenzi ya mafunzo pamoja na kamati ya usajili na mitihani ya Baraza la madaktari wa Tanganyika (MCT), wamefanya kikao cha pamoja katika ukumbi wa TNMC Jijini Dodoma, ambapo kamati ya mitihani ya Baraza la Madaktari ilifika ofisi za Baraza la Uuguzi na Ukunga kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu wa jinsi ya uendeshaji na uratibu wa mitihani ya usajili na leseni.

Akifafanua kwa undani juu ya lengo la kikao hicho Mkurugenzi wa mafunzo na maendeleo ya taaluma wa TNMC Bi. Happy Masenga, amesema, wajumbe wa kamati ya mitihani ya MCT wamefika katika Ofisi za TNMC ili kujifunza namna TNMC inavyoratibu, na kuendesha Mtihani jinsi ambavyo TNMC imefanikiwa kuratibu ufanyikaji wa mitihani hiyo sanjari na mitihani ya Taifa ya kada za Afya za kati inayoratibiwa na Idara ya mafunzo na maendeleo ya wataaluma.

***"Maeneo mengine waliojifunza ni pamoja na; Uandaaji Maswali (Item Development) Uchambuzi wa maswali (Item Moderation)***



***kupangilia karatasi ya maswali (Paper Setting) Kuzalisha, kupaki na kuitunza karatasi za mitihani (Paper printing, packing and storage)"*** Alisema Mkurugenzi Masenga

Akizungumzia hatua za maandalizi ya mtihani, amesema katika kila hatua ya maandalizi ya mtihani, timu au kikosi kazi cha kuratibu zoezi hilo kinakuwa kimetambuliwa ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji wa vyombo vya usalama ili kuhakikisha kila hatua ya zoezi inafanyika kwa kuzingatia Sheria na miongozo, lakini pia maandalizi ya vituo vya mitihani yanafanyika kwa kuzingatia maoteo ya idadi ya watahiniwa wanaotarajiwa kufanya mtihani katika awamu husika.

Aidha, wajumbe walihudhuria kikao hicho kwa Upande wa MCT ni pamoja na Dkt. Deusdedith Ndilanha - Mwenyekiti wa Kamati Dkt. Elizabeth Mrema - Mratibu wa Mitihani Dkt. Elisha Osati - Mjumbe wa Kamati Dkt. Larry Akoko - Mjumbe wa Kamati.

Kutoka TNMC ni pamoja na Kurugenzi wa Mafunzo ni Bi. Happy Masenga, Setberth Haramba, Mratibu wa Mitihani, Kafumu John na Bi. Mwajuma Mutabazi ambao ni waratibu wa mafunzo

# "Leseni Kwa Muuguzi, Mkunga ni Kibali Cha Utoaji Huduma" - Bi. Jane Mazigo.

Na. Ezekiel Nyalusi

***"Leseni ni utambulisho kwa muuguzi na mkunga kutoa huduma kwa jamii na ipo kwa mjibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 hivyo, ni vyema kwa Muuguzi na Mkunga kuwa na leseni iliyo hai muda wote wa kutoa huduma".***

Hayo ameyasema Bi. Jane Mazigo, Mkurugenzi wa Maadili, Usajilina Leseni akizungumza na TNMC Habari mapema tarehe 19 septemba 2024.

Bi. Mazigo, ameongeza kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga kifungu cha 21 (a) na (b) Sheria inafafanua majukumu ya msajili wa TNMC kuwa ni kumsajili Muuguzi na Mkunga na kumpa leseni pamoja na kuhuisha leseni hiyo mara inapokwisha muda wake kwa mujimu wa miongo ya Baraza.




***"pia kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga kifungu cha 38 inaeleza adhabu ambazo muuguzi na mkunga atakumbana nazo pindi atakapobainika akitoa huduma pasipo kuwa na leseni hai"*** alisema Bi.Mazigo

Katika hatua nyingine Bi.Mazigo, amewakumbusha waajiri wa wauguzi na wakunga kote nchini, kuhakikisha wanazingatia leseni kwa wataaluma hao kabla ya kuwaajiri kwani ni kosa kisheria

Zaidi ya wauguzi 6,000 wanatakiwa kuhuisha leseni zao katika kipindi cha kuanzia tarehe 01 Julai mpaka 30 Disemba 2024 kwa gharama za kawaida na baada ya muda huo kupita mfumo utaanza kutoza pamoja na penati, hivyo wauguzi wote mnaofahamu kuwa mnatakiwa kuhuisha leseni ni vema mkatumia muda ulibainishwa kuhuisha leseni zenu pasipo kusahau kuwa na alama muhimu za kujiendeleza kitaaluma yaani CPD Point.






# TNMC Kuanzisha Kituo Cha Mawasiliano, Kuboresha Utoaji Huduma Kwa Mteja.

## Sasa Kutumia Namba Moja Maalum

Na. Mwandishi wetu

Katika kuboresha huduma kwa mteja, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) linaendelea na mchakato wa kuanzisha kituo cha mawasilino na wadau wake hususani wauguzi na wakunga nchini na duniani kwa ujmla, machakato ambao unatarajiwa kukamilika na kuanza kutumika mapema mwezi huu Oktoba 2024.

TNMC inajenga mfumo huu wa mawasiliano baada ya kuwepo kwa changamoto kadhaa kwa mfumo wa sasa ambao mtu yeyote anayewasiliana na Baraza analazimika kutumia namba binafsi za Maafisa waliopo kwenye kurugenzi na vitengo kushugulikia masuala mbalimbali kama vile usajili na leseni, Mitihani, Indexing na majukumu ya jumla ya Baraza.


Mapema Septemba 19, 2024 mtaalamu kutoka kampuni ya simu ya TTCL alitoa mafuzo kwa maafisa wa TNMC yaliyolenga kuwajengea uwezo wa namna ya kuutumia Mfumo wakati wa kuwasiliana, miongoni mwa mambo mazuri na ya msingi yaliyofundishwa ni pamoja na Mawasiliano hayo kutumia kompyuta mpakato badala ya simu na wateja zaidi ya watano wanaweza kupiga



simu kwa kutumia namba moja maalum itakayoteuliwa ambapo, mteja anaweza kuipiga kupitia mtandao wowote.

Mfumo utakuwa na uwezo wa kumuelekeza mpigaji Ofisi sahihi ya kushughulikia huduma anayohitaji, mfumo utakuwa na uwezo wa kurekodi mazungumzo ya Mteja na Mtoa huduma kwa ajili ya rejea, lakini pia mfumo huu wa mawasiliano utakuwa na uwezo wa kumwelekeza mtoa huduma jinsi ya kutatua changamoto anazokutananazo Mfano. Namna ya kutengeneza Nywila (Password) kwa waliosahau pasipo kuongea na mtoa huduma.

TNMC kupitia mkataba wake wa huduma kwa wateja, mara zote imedhamilia kutoa huduma bora kwa umma hususani wauguzi na wakunga wanapofika ofisini au kwa njia ya mawasiliano kwa shabaha ya kudumisha uhusiano chanya jambo ambalo litachangia jamii ipate huduma bora na salama.



# Ufahamu Ugonjwa wa MPOX na Athari zake kwa Jamii

## MPOX ni nini?

Ugonjwa wa Mpox husababishwa na virusi vya monkeypox, familia moja ya virusi na ndui, ingawa si kali sana.
Virusi hivi awali vilisambazwa kutoka kwa wanyama hadi kwa wanadamu, na hupatikana zaidi katika nchi zilizo karibu na misitu ya mvua ya kitropiki.

Katika maeneo hayo, kuna maelfu ya wagonjwa na mamia ya vifo kutokana na ugonjwa huo kila mwaka, na watoto chini ya umri wa miaka 15 wameathirika zaidi.





## Je, Hueneaje?

Mpox huenea kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine kwa kuwa karibu na mtu aliyeambukizwa, ikiwa ni pamoja na kupitia ngono, kugusana ngozi au kupumua karibu na mtu mwingine.

Virusi vinaweza kuingia mwilini kupitia macho, pua au mdomo.

kupitia ngozi iliyo na michubuko, njia ya upumuaji au Inaweza pia kuenea kwa kugusa vitu ambavyo vilishikwa au kutumiwa na mwenye virusi, kama vile matandiko, nguo na taulo.

Kugusana kwa karibu na wanyama walioambukizwa, kama vile nyani, panya na Kuchakuro (squirrels), ni njia nyingine.



## Je, inawezaje kutibiwa?

Tiba iliyoundwa kutibu ndui inaweza pia kuwa muhimu katika kutibu mpox, lakini kuna utafiti mdogo kuhusu jinsi inavyofaa.

Milipuko ya mpox inaweza kudhibitiwa kwa kuzuia maambukizi, njia bora ya kufanya hivyo ni kwa chanjo.

Kuna chanjo tatu ambazo zipo lakini ni watu walio hatarini tu au ambao wamewasiliana kwa karibu na mtu aliyeambukizwa kwa kawaida wanaweza kuipata.

Hata hivyo, Shirika la Afya Ulimwenguni WHO linashauri kuwa kwa sasa haipendekezi kuchanja watu wote.

Bado majaribio zaidi ya chanjo dhidi ya aina mpya za mpox yanahitajika ili kuelewa ni kiasi gani cha ulinzi kinachotoa.


Chanzo: BBC SWAHILI

# Tanzia

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limepokea kwa Masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele ya haki Mwezi Septemba, 2024, baada ya kumaliza kazi ya hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao Mahali pema Peponi AMENI.



JINA: GAUDENCE GILAGIZA
KITUO: Ilembula school of Nursing
MKOA: Njombe
WILAYA: Wanging'ombe



JINA: SPONSOR MBILINYI
KITUO: Kituo cha Afya Buguruni
MKOA: Dar es Salaam
Halmashauri: Kinondoni



JINA: JAMES BUETTA
KITUO: Zahanati ya Olele
MKOA: Kilimanjaro
WILAYA: Arusha



JINA: VUMILIA MKINI
KITUO: Zahanati ya Mdandu
MKOA: Njombe
WILAYA: Wanging'ombe



JINA: JOSEPH BUNDALA
KITUO: Zahanati ya Mgubike
MKOA: Morogoro
WILAYA: Kilosa



JINA: THEONESSTINA RWECHUNGURA
KITUO: Hospitali ya Nyamagana
MKOA: Mwanza
WILAYA: Nyamagana

JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
S.L.P 1736 DODOMA , **Simu:0737-96-26-91**
Barua Pepe:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA